

TANGAZO

26/03/2018

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inawatangazia wananchi wote kwa ujumla kuwa zoezi la uhakiki wa vyeti vya kuhitimu Kidato cha Nne, Sita Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa watumishi wote linaendelea kwa wale ambao kwa namna moja ama nyingine hawakuweza kuwasilisha nakala za vyeti vyao kwa ajili ya kuhakikiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Kwa kuwa zoezi hili linahitaji ushirikiano wa hali ya juu na wadau mbalimbali Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) inaomba kama kuna mwananchi au mtumishi yoyote mwenye taarifa za watumishi ambao hawajafanyiwa uhakiki au anamjua mtumishi mwenye cheti cha kughushi lakini bado yupo kwenye Utumishi wa Umma, atoe taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) au namba ya simu 027 - 2977306 taarifa hizo zitakuwa za **SIRI**.

Tangazo hili limeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) – Kilindi.

Nashukuru kwa ushirikiano wenu



Edward Mhina

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KILINDI**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KILINDI**